

## 05- Faida za Elimu ya Tajwiyd

Tajwiyd ni nuru ya Qur-aan, na pambo la kila Aayah, bali mahadhi yake ni miujiza ya Qur-aan kwani mwenye kuisoma huzidi kuipenda na kuwa ni furaha yake ya moyo na hupata utulivu yeye na anayemsikiliza. Kuisoma Qur-aan ipasavyo ni poza ya dhiki na maradhi ya moyo na ya mwili na hidaaya kamilifu kwa binaadamu, kwani haya sio maneno ya mtu bali ya Mwenyewe Allaah (سبحانه وتعالى), Muumba wa roho na mwili wa binaadamu. Ndipo Anaposema Allaah (سبحانه وتعالى):

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا<sup>١</sup> مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا الْكِتَابُ وَلَا الْإِيمَانُ وَلَٰكِن جَعَلْنَاهُ  
نُورًا نَهْدِي بِهِ<sup>٢</sup> مَن نَّشَاءُ مِنْ عِبَادِنَا<sup>٣</sup>

**((Na hivyo ndivyo Tulivyokuletea Ruwh katika Amri Yetu. Hukuwa unaelewa nini Kitabu, na wala (nini) iymaan, lakini Tumeijaalia (kuwa) ni Nuru, Tunamhidi kwayo Tumtakaye kati ya waja Wetu))<sup>1</sup>**

Allaah (سبحانه وتعالى) Ameiita hii Qur-aan ni 'roho' kwa sababu roho ndio inayohuisha mwili. Na Qu-raan inahuisha pia nyoyo, na inahuisha pia maslahi ya dunia na ya Dini ambayo ina kheri nyingi na elimu tukufu.<sup>2</sup>

Hakika asiyeisoma Qur-aan kwa Tajwiyd amenyimwa utamu wa kusoma Qur-aan na fadhila zake tukufu.

Baadhi ya faida za kuwa na elimu ya Tajwiyd ni:

### 1-Kuwa pamoja na Malaika Watukufu

عَنْ عَائِشَةَ (رضي الله عنها) عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((مَثَلُ الَّذِي يَقْرَأُ الْقُرْآنَ وَهُوَ حَافِظٌ لَهُ  
مَعَ السَّفَرَةِ الْكِرَامِ الْبَرَّةِ وَمَثَلُ الَّذِي يَقْرَأُ وَهُوَ يَتَعَاهَدُهُ وَهُوَ عَلَيْهِ شَدِيدٌ فَلَهُ أَجْرَانِ))

**Imetoka kwa 'Aaishah (رضي الله عنها) kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema:  
((Yule aliyekuwa hodari wa kusoma Qur-aan atakuwa pamoja na**

<sup>1</sup> Ash-Shuwraa (42: 52)

<sup>2</sup> Tafsiyr Imaam As-Sa'dy

Malaika Waandishi [wa Allaah] watukufu wema, na yule ambaye anaisoma Qur-aan kwa mashaka na huku anajitahidi kwa kudodosa atapata ujira mara mbili)<sup>3</sup>

## 2-Hupendwa kusikilizwa Qiraa-ah Chake

Ingawa Qur-aan iliteremshwa kwake Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipenda kumsikiliza mtu mwingine aisome. Alifurahishwa na qiraa-ah cha Abu Muwsaa Al-Ash'ariyy (رضي الله عنه) siku moja alikaa kumsikiliza:

عَنْ أَبِي مُوسَى الْأَشْعَرِيِّ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ لَهُ: ((لَوْ رَأَيْتَنِي وَأَنَا أَسْتَمِعُ لِقِرَاءَتِكَ الْبَارِحَةَ لَقَدْ أُوتَيْتَ مِزْمَارًا مِنْ مِزَامِيرِ آلِ دَاوُدَ))

Kutoka kwa Abu Muwsaa Al-'Ash'arriy (رضي الله عنه) kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) kamwambia: ((Ungeliniona jana nilivyokuwa nakusikiliza kisomo chako. Hakika umepewea mizumari miongoni mwa mizumari ya aila ya Daawuwd))<sup>4</sup>

## 3- Imaam Wa Swalah

Maimaam waliohifadhi Qur-aan, hupewa fadhila ya kuongoza Swalah haswa yule mwenye elimu zaidi ya Qiraa-ah.

عَنْ أَبِي مَسْعُودٍ الْأَنْصَارِيِّ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ((يَوْمَ الْقَوْمِ أَقْرَأُهُمْ لِكِتَابِ اللَّهِ فَإِنْ كَانُوا فِي الْقِرَاءَةِ سَوَاءً فَأَعْلَمُهُمْ بِالسُّنَّةِ فَإِنْ كَانُوا فِي السُّنَّةِ سَوَاءً فَأَقْدَمُهُمْ هِجْرَةَ فَإِنْ كَانُوا فِي الْهِجْرَةِ سَوَاءً فَأَقْدَمُهُمْ سَلْمًا وَلَا يُؤْمَنُ الرَّجُلُ الرَّجُلَ فِي سُلْطَانِهِ وَلَا يَقْعُدُ فِي بَيْتِهِ عَلَى تَكْرِمَتِهِ إِلَّا بِإِذْنِهِ))

Kutoka kwa Abu Mas'uud Al-Answaariyy (رضي الله عنه) amesema: Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: ((Awaswalishe watu yule mwenye kujua kusoma zaidi Kitabu cha Allaah na wakiwa katika kusoma wako sawa, basi mwenye ujuzi zaidi wa Sunnah, na wakiwa kwenye Sunnah wako sawa, basi aliyetangulia Hijrah, na wakiwa katika hijrah wako sawa, basi mkubwa wao kwa umri, wala asiswalishe mtu (mwingine) katika nyumba yake

<sup>3</sup>Al-Bukhaariy na Muslim

<sup>4</sup>Muslim

wala katika mamlaka yake wala asikae mahali pake pa heshima isipokuwa kwa idhini yake)))<sup>1</sup>

Wangapi wanakwenda masafa mbali kufuata msikiti wenye Imaam mwenye kuswalisha kwa *qiraa-ah* kizuri hasa katika mwezi wa Ramadhaan wakati Qur-aan nzima inakhitimishwa misikitini.

Wangapi wanaopata uongofu na iymaan zao kuzidi kwa kusikia Qur-aan ikisomwa kwa kufuatwa hukmu zake za Tajwiyd ambazo ndizo zinazosababisha *qiraa-ah* kuwa kizuri?

Wangapi wasio Waislamu wamevutiwa na Qur-aan inaposomwa vizuri bila hata ya kujua maana yake, hatimaye wakasilimu?

Hakika elimu ya Tajwiyd ni hazina ya thamani kuu duniani na Akhera, kwa hiyo, kila anayetamani kuwa na hazina hii ajifunze hukmu za Tajwiyd, somo ambalo ni jepesi kwa mwenye utashi (nia na hima) nalo na kutilia juhudi.